# WWF ilivyodhamiria kushirikiana na serikali kutokomeza ujangili ushoroba wa Selous na Niassa

**Na Albano Midelo**

SHIRIKA la kimataifa la WWF limedhamiria kuhakikisha ushoroba wa wanyamapori kutoka Pori la Akiba la Selous,kupitia Pori  la Liparamba hadi hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji,unalindwa kikamilifu dhidi ya majangili.



Mratibu Msaidizi wa Uwanda wa Ruvuma Mhifadhi,Asukile Kajuni amesema wamejipanga kuulinda ushoroba huo kufuatia utafiti uliofanywa na  Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori TAWIRI mwaka 2009,kubaini kasi ya ujangili wa wanyamapori nchini inatishia wanyama adimu kutoweka.

Kulingana na utafiti huo,ifikapo mwaka 2050, huenda zitabaki hifadhi za Ruaha na Pori la Akiba la Selous ,endapo hatua za makusidi hazitachukuliwa kukabiliana na ujangili wa wanyamapori nchini.

Meneja wa Mawasiliano wa Shirika la WWF Joan Itanisa amesema wafanyakazi wa WWF hawaingia porini kukimbizana na majangili ,badala yake wanafanya uhamasishaji na kampeni maalum ya kuhakikisha vita ya kupambana na ujangili wa tembo katika pori la Selous ili pasiwepo na tembo hata mmoja anayeuawa.




Katika kuhakikisha vita hiyo inafanikiwa Itanisa amesema WWF ina  wahifadhi ambao wapo vijijini (Village Game Scouts) ambao wamekuwa wanasaidiwa kupata elimu ya uhifadhi katika Chuo cha Uhifadhi cha Likuyu Sekamaganga wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma,ili kusaidia katika mapambano hayo.

“Wahifadhi hao wanasomeshwa na WWF kwa miezi mitatu katika chuo hicho,pia baada ya mafunzo wanapewa vifaa vya kufanyia kazi na vitu vingine ili kupambana katika vita hii”,anasema Itanisa.

Hata hivyo Meneja huyo wa Mawasiliano wa WWF anasema askari wa wanyamapori wanafanyakazi kwa karibu na shirika hilo ambapo WWF imekuwa inawapa elimu na vifaa ambapo Julai mwaka huu wakati wa maadhimisho ya siku ya wanyamapori kitaifa,WWF iliweza kutoa vifaa  vyenye thamani ya shilingi milioni 110.

WWF ilianzishwa mwaka 1961,makao makuu yake yapo nchini Uswiss ,Shirika hilo linafanyakazi katika nchi zaidi ya 100 duniani,katika bara la Afrika WWF ina ofisi katika nchi kumi ikiwemo Tanzania.

Kulingana na Meneja huyo,WWF ilianza kufanyakazi hapa Tanzania mwaka 1990 na kwamba inatekeleza miradi sita ukiwemo mradi wa kuhifadhi wanyamapori ambao umesimamia kuhifadhi wanyamapori wakubwa wawili ambao ni tembo na faru ambao wapo katika hatari ya kutoweka.

Amesema katika ukanda wa Selous miaka michache iliyopita kulikuwa na wimbi kubwa la ujangili ambao ulisababisha asilimia 90 ya tembo katika pori la Selous kuuawa na kwamba hali hiyo ndiyo imelisukuma shirika la WWF kushirikiana na serikali kupambana na ujangili.

“Tumefanya kampeni kubwa na maalum katika kipindi cha miaka miwili ya kuhifadhi tembo wa Selous,ambapo hivi sasa matukio ya ujangili yamepungua kwa kiasi kikubwa katika ushoroba wa Selous-Niassa na tembo wameanza kuongezeka”,anasisitiza Itanisa.



Kwa upande wake Mkuu wa Kampeni ya kuzuia ujangili dhidi ya tembo wa WWF, Atilio Tagalile ameipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kuimarisha vita dhidi ya ujangili wa tembo kwenye pori la Selous ambapo hivi sasa ujangili umepungua kwa kiwango kikubwa.

“Hapo awali katika pori la Selous kwa siku walikuwa wanauawa tembo hadi 15,lakini hivi sasa matukio yamepungua unaweza kuona mizoga ya tembo wasiozidi wawili,kwa kweli serikali hii inastahili pongezi”,anasisitiza Tagalile.

Amesema miaka 1970 idadi ya tembo katika pori la Akiba la Selous ilifikia zaidi ya 110,00 na kwamba majangili waliua tembo kwa asilimia 90 na kusababisha wanyama hao katika pori hilo kuwa katika hatari ya kutoweka.

Hata hivyo Meneja wa Mawasiliano katika Mamlaka za Usimamizi wa wanyamapori nchini (TAWA) Twaha Twalibu amesema ujangili dhidi ya tembo unaendelea kudhibitiwa ambapo hivi sasa katika hifadhi na mapori likimo pori la Selous idadi ya tembo inaongezeka kwa kasi.

Pori la akiba la Selous ni moja kati ya vivutio vikubwa vya utalii hapa nchini na endapo lingetangazwa kwa nguvu zote lingeweza kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na kuongeza pato la taifa.

Selous ni moja kati ya mapori 28 ya Akiba hapa nchini yaliyopo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania(TAWA).

Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 ambazo sawa na asilimia tano ya ardhi yote ya Tanzania Bara linaangukia katika mikoa minne na wilaya kumi.

Mikoa hiyo kwa mujibu wa Meneja wa Pori la Akiba la Selous Mhifadhi Henock Msocha ni Ruvuma, Lindi,Pwani na Morogoro na wilaya ambazo zinapita katika Pori hilo ni Liwale, Kilwa, Rufiji, Kilombero, Morogoro vijijini, Malinyi, Namtumbo, Tunduru na Kisarawe.




Selous ni moja kati ya mapori mengi yaliopo hapa nchini likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 likijumuisha maeneo ya ardhi oevu,misitu ya miombo,tambarare ,nyasi za kuvutia,maziwa na mito inayotiririka na kuwa kivutio.

Msocha anabainisha zaidi kuwa kutokana na ukubwa wa pori hilo,limegawanywa katika kanda nane ili kurahisisha shughuli za usimamizi na utendaji kazi.

Anazitaja kanda hizo kuwa ni Kanda ya Kaskazini (Matambwe),Kanda ya Kaskazini Mashariki (Kingupira),Kanda ya Mashariki(Miguruwe), Kanda ya Kaskazini Magharibi (Msolwa), Kanda ya Kusini Mashariki(Liwale), Kanda ya Kusini (Kalulu), Kanda ya Kusini Magharibi(Likuyusekamaganga) na Kanda ya Magharibi(Ilonga).

Pori la Akiba la Selous lilianzishwa mwaka 1896 na Wajerumani likiwa pori la kwanza kutengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori barani Afrika na la pili kwa ukubwa duniani baada ya pori la Marekani ambalo linaitwa Yellowstone National Park.

Historia inaonesha kuwa jina la Selous limetokana na askari ambaye alikuwa ni mvumbuzi wa kiingereza aliyeitwa kapteni Fredrick Selous aliyefariki Januari 4, mwaka 1917 wakati anapigana vita ya pili ya Dunia na kuzikwa katika eneo la Behobeho lililopo ndani ya pori la Selous .

Pori la Akiba Selous lina utajiri wa viumbe adimu katika sura ya dunia kama vile nyani aina ya sanje,mbega mwekundu,faru mweusi ambaye yupo hatarini kutoweka na wanyama wengine wakiwemo ndege,wadudu na mimea ambayo haipatikani sehemu nyingine yeyote duniani.

Kutokana na umuhimu wa pori la Selous Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Utamaduni na Sayansi (UNESCO) limelihorodhesha pori hilo kuwa ni moja ya maeneo ya asili ya urithi wa dunia tangu mwaka 1982.



Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anasema Pori la Selous lenye idadi kubwa ya tembo ni mapito ya wanyama yaani ushoroba wa tembo ambao wanatoka katika pori hilo kupitia pori la Akiba la Liparamba na kuingia hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji.

“Selous ndiyo pori la Akiba linalosifika kuwa na uoto wa kuvutia wa miombo na idadi kubwa ya wayama aina ya tembo hali inayosababisha wakati mwingine wanyama hao kutoka nje ya pori na kwenda katika makazi ya watu na kusababisha uharibifu wa mali”,anasema Challe.

Takwimu zinaonesha kuwa katika pori hilo hadi kufikia mwaka 2007 kulikuwa na tembo zaidi ya 70,000 hata hivyo idadi ya tembo katika pori hilo ilishuka kutokana na kukithiri kwa ujangili kwa asilimia 90.

Meneja wa Pori hilo Henock Msocha anasema ili kuhakikisha ujangili unadhibitiwa katika pori hilo,inafanyika doria ndefu na fupi katika kanda zote nane na kwenye maeneo ya pembezoni.

“Vikosi vyenye askari sita vimeundwa katika kila Kanda kwa ajili ya kutekeleza kazi za doria kwa kupishana na hivyo kuhakikisha kuwa pori lipo chini ya ulinzi wakati wote”,anasisitiza Msocha.

Anaongeza kuwa doria za ushirikiano zimefanyika kwa kuhusisha askari wa Pori la Akiba Selous na askari wa Halmashauri za Wilaya zinazozunguka pori hilo kwa kushirikiana na askari wa kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU),Wakala wa Misitu(TFS) na Jeshi la polisi.

Mafanikio ambayo tayari yamepatikana katika uwindaji wa kitalii kupitia pori hilo ni pamoja na Tanzania kufikiwa na watalii wawindaji 662 katika pori hilo mwaka 2005,mwaka 2006 watalii 437 na mwaka 2007 watalii 549.

Kulingana na Msocha katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Juni 2017 jumla ya doria 2179 zilitekelezwa na kwamba ongezeko la doria hizo limetokana na uboreshaji wa miundombinu ya doria na vitendeakazi ikiwemo ongezeko la magari kwa ajili ya doria.



“Katika kipindi hicho tumekamata jumla ya majangili 520 kwa makosa mbalimbali kinyume cha sheria ya kuhifadhi wanyamapori na kanuni zake,vitendo hivyo vinajumuisha kuingia ndani ya pori bila kibali,kuwinda wanyamapori bila kibali,kutega wanyama,kuvua samaki na kuingiza mifugo na uvunaji haramu mazao ya misitu”,anasema Msocha.

Anaongeza kuwa katika kipindi hicho walikamata vifaa mbalimbali vya kufanyia ujangili ikiwemo bunduki 20 za aina mbalimbali,roda 747 za kutegea wanyama, pikipiki 14,magari mawili,baiskeli 59,misumeno ya kuchania mbao 16,mikuki tisa,nyavu za kuvulia samaki 204 na mitumbwi 106.

“Juhudi hizi zimewezesha kudhibiti vitendo vya ujangili katika kiwango kikubwa,hali iliyosababisha matukio ya vifo vya tembo kutokana na ujangili yamepungua kutoka tembo 17 mwaka 2015/2016 hadi kufikia tembo wanane mwaka 2016/2017”,anasema Msocha.

**Mwandishi ni Mchangiaji wa gazeti hili,mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**
**Novemba 14,2018**